**Mix By Yas**

- Piga *150*01#
- Chagua 4 Lipa Bili
- Chagua 5 Malipo ya Serikali
- Chagua 1 ingiza namba ya malipo
- Weka kiasi
- Chagua 2 ingiza kiasi
- Weka namba ya siri kuthibitisha
- Utapokea ujumbe unaokujulisha malipo
- yamekamilika

**Airtel**

- Piga*150*60#
- Chagua 5 Lipa Bill
- Chagua 5 Malipo ya Serikali
- Chagua 1 Ingiza control number
- Ingiza kiasi cha pesa
- Weka namba ya Siri kulipia
- Utapokea ujumbe utakaokujulisha ombi lako
- linashughulikiwa.

**TTCL**

- Piga *150*71#
- Chagua 4 Lipa bili
- Chagua 6 Malipo ya Serikali
- Weka namba ya kumbukumbu
- Weka kiasi
- Ingiza namba ya siri kuthibitisha malipo
- Utapokea ujumbe unaokujulisha malipo
- yamepokelewa

### Je nitaitumiaje kadi yangu?

Gusisha kadi yako kwenye sehemu yenye alama ya mkono ulioshika kadi kwenye geti janja mpaka litakapokuonesha alama na sauti ya kukuruhusu kupita.

### ZINGATIA

Ukishagusisha kadi yako kwenye geti la kuingia kituoni, mara linapokuruhusu kuingia unapaswa kutumia chini ya sekunde 8 kupita, vinginevyo geti litajifunga na halitokuruhusu kuingia tena.

## Jinsi ya kuisajili kadi yako ya Mwendokasi kupitia Mwendokasi App

Mfumo wa Ukusanyaji Nauli wa Serikali katika Mabasi Yaendayo Haraka ujulikanao kama Automated Fare Collection System (AFCS) umetoa fursa kwa abiria kuunganisha kadi yake ya Mwendokasi na App ya Mwendokasi ili kumrahisishia kuona taarifa mbalimbali za kadi yake kwa mfano;

1. Kuona taarifa ya vituo ulivyovitumia kuchanja Kadi yako.
2. Kuona tarehe ulizosafiri
3. Kuona muda (Saa) ulipoingia Kituoni
4. Kona kiasi cha nauli ulichokatwa
5. Kuona salio lililobaki baada ya kukatwa kiasi cha nauli
6. Vilevile utaweza kuona historia ya miamala uliyoifanya baada ya kuweka salio kwenye kadi yako.

### Ili kuunganisha Kadi yako ya Mwendokasi na Mwendokasi App fuata hatua zifuatazo;

1. Fungua Mwendokasi App kwenye Simu Janja yako
2. Kwenye Menu chini, bonyeza kadi
3. Kisha bonyeza "Add Card"
4. Utaweka namba yako ya kadi
5. Itakuletea ujumbe "Ingiza OTP" ambayo itatumwa kwenye namba yako ya
6. simu uliyoitumia kusajilia kadi
7. App itafunguka kwenye sehemu iliyoandikwa Card zangu, hapo Utaweza kuona taarifa ya vituo ulivyotumia kuchanja kadi yako, tarehe na muda uliotumia, kiasi ulichokatwa na kiasi kilichobaki kwenye kadi yako
8. Historia ya miamala, utaona historia ya miamala uliyoifanya

### NIFANYE NINI ENDAPO KADI YANGU ITAKUWA IMEPOTEA?

Iwapo utakuwa umepoteza kadi yako, abiria utahitajika kutoa taarifa kwa kupiga simu kupitia namba za Huduma kwa Wateja 0800110147 (Bure) ukiwa na namba ya kadi yako ya Mwendokasi pamoja na taarifa zako za muhimu ambazo zitahitajika na Maafisa wa DART.

Baada ya hapo utahitajika kufika kwenye Ofisi za Wakala wa Mabasi Yaendaqyo Haraka na kiasi cha Shilingi 5000/= pamoja na Kitambulisho ulichotumia kusajilia kadi yako.

### WASILIANA NASI

**WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA**
**Ubungo Maji, Morogoro Road**
**S.L.P 724, 16103 Dar es Salaam**
**Simu: +255 222928634/33**
**Fax: +255 222 92 8635**
***Email:info@dart.go.tz***

@DARTMwendokasi DARTTV Simu ya Bure 0800 110 147




# ZINGATIO KWA ABIRIA WA MWENDOKASI

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wanawatangazia abiria wa Mabasi Yaendayo Haraka maarufu Mwendokasi, kuendelea kununua na kutumia Kadi Janja za Mwendokasi.**

**Matumizi ya Kadi Janja yanasaidia Serikali kuepuka upotevu wa mapato hivyo tunawahamasisha watumiaji abiria wote wa Mwendokasi kutumia kadi. Aidha, kuanzia tarehe 01 Juni 2025 matumizi ya tiketi za karatasi zenye alama ya msimbo kodi zitasitishwa hivyo ni vyema kila mmoja ajipatie kadi janja yake ya Mwendokasi.**

DART
DAR RAPID TRANSIT AGENCY

# KADI YA MWENDOKASI

Hii ni Kadi Janja ya kielektroniki ambayo hutumika kulipia nauli katika Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Kadi ya Mwendokasi ina ubora wa hali ya juu na ina uwezo wa kupokea kadi nyingine.

- Kadi hii inatumia teknolojia ya NFC (Near Field Communication) yaani unaweza kuitumia hata ikiwa ndani ya wallet, mradi tu iwe na salio na uigusishe kwenye kihakiki kadi kwenye geti janja la Mwendokasi.
- Muonekano wa kadi hii upande wa mbele kuna Namba ya Malipo (Control Number au Kumbukumbu Namba) ambayo ni namba ya Utambulisho wa Kadi kwa abiria na itakuwezesha kuitumia wakati wowote unapoongeza salio kwa ajili ya nauli kwenye Huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Aidha kwa upande wa nyuma wa kadi unatoa fursa kwa wawekezaji na wafanyabiashara kutangaza huduma na bidhaa zao kwa gharama nafuu na kuwafikia wateja wengi zaidi.

## FAIDA ZA KADI YA MWENDOKASI

- Ni rafiki kwa utunzaji wa mazingira
- Hakuna haja ya kubeba pesa taslimu
- Inaokoa muda kwa kumuepusha abiria kusimama kwenye foleni ya ukataji wa tiketi za karatasi zenye alama ya Msimbokodi pamoja na kusubiria chenji.
- Inamrahisishia mtumiaji kupanga bajeti ya matumizi
- kwenye usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka.
- Inadhibiti uvujaji wa mapato.

## NINAWEZAJE KUPATA KADI YA MWENDOKASI?

Kwa sasa Kadi ya Mwendokasi inapatikana kwenye Vituo Vikuu (Terminals) na Vituo vidogo vya Mabasi Yaendayo Haraka kwa gharama ya Sh. 5000/= ikiwa na salio ndani yake la Sh. 3000/= linakuwezesha kuanza kuitumia papo hapo baada ya kuisajili.

Kadi Janja za Mwendokasi kwa hivi sasa zinapatikana katika Kituo Kikuu cha Kimara, Kivukoni, Gerezani na Morocco. Vilevile zinapatikana katika Kituo cha Korogwe, Halmashauri ya Jiji, na Msimbazi B.

## Ni viambatanisho vipi ninapaswa kuwa navyo ili niweze kusajili Kadi ya Mwendokasi?

Ili uweze kusajili na kupata kadi hii unapaswa kuwa na Kitambulisho au namba ya Nida, Kitambulisho cha Mpiga Kura, Hati ya Kusafiria, Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

## Ni namna gani naweza kuweka salio katika Kadi ya Mwendokasi?

Unaweza kuongeza salio kwenye kadi hii kupitia dirisha la kuuzia tiketi kwenye vituo vya Mabasi Yaendayo Haraka. Aidha kutokana na kukua kwa teknolojia, malipo ya kabla ya nauli ya Mabasi Yaendayo Haraka kupitia kadi janja ya Mwendokasi yanaweza kufanyika kwa kuhamisha salio kutoka E-Wallet ya Mwendokasi App, kupitia miamala ya simu kama vile M-Pesa, Mix By Yas, Airtel Money, Halotel, T-Pesa na miamala ya Kibenki kama vile NMB na NBC.

## Hatua za kuhamisha salio kutoka E- Wallet ya Mwendokasi App kwenda kwenye Kadi

1. Fungua Programu Tumizi ya Mwendokasi (Mwendokasi App) katika simu janja yako.
2. Bofya kitufe lichoandikwa 'Kata tiketi'.
3. Ingiza namba ya siri kuthibitisha akaunti yako.
4. Bofya kitufe cha 'Hamisha salio'.
5. Chagua kitufe cha 'Hamisha kwenda kwenye Kadi'.
6. Andika namba ya kadi ya yule unayemuhamishia salio halafu weka kiasi kisha bofya kitufe cha 'Tuma taarifa'.
7. Hakiki taarifa ya Jina la mpokeaji, Namba ya kadi na Kiasi halafu bofya neno 'Tuma'.
8. Thibitisha taarifa za uhakiki wako kwa kubofya neno 'Ndio'.
9. Utapokea ujumbe kukujulisha muamala umefanikiwa.




## Jinsi ya kuweka salio kwenye Kadi ya Mwendokasi kwa abiria anayetumia Benki ya NBC

- Piga *150*55#
- Weka neno lako la Siri kuendelea
- Chagua 2 Lipa bili
- Weka 1 chagua Kampuni
- Bonyeza ## kuendelea
- Chagua 4 Malipo ya Serikali
- Ingiza Namba ya Malipo
- Weka kiasi
- Bonyeza 1 kuthibitisha
- Utapokea ujumbe kukuarifu malipo yamekamilika

NBC National Bank of Commerce Conveniently Everywhere.

## Jinsi ya kuweka salio kwenye Kadi ya Mwendokasi kwa abiria anayetumia huduma ya NMB Mkononi

- Piga *150*66#
- Chagua 2 Lipa Bili
- Chagua 3 Serikali
- Ingiza Namba ya Malipo
- Weka 1 Lipa
- Ingiza kiasi kisichopungua TZS 1
- Ingiza PIN ya NMB Mkononi
- Weka 1 kuthibitisha
- Utaletewa ujumbe ombi lako limepokelewa

NMB

## JINSI YA KUWEKA SALIO KWENYE KADI YA MWENDOKASI KUPITIA MITANDAO YA SIMU

### Halotel

Piga *150*88#
Chagua 4 Lipa bili
Chagua 5 Malipo ya Serikali
Ingiza kumbukumbu namba
Ingiza Kiasi
Ingiza PIN
Bonyeza 1 kuthibitisha
Utapokea ujumbe utakaokujulisha malipo ya muamala yanafanyiwa kazi.

halopesa

### Vodacom

Piga *150*00#
Chagua 4 Lipa kwa M-Pesa
Chagua 5 Malipo ya Serikali
Chagua 1 weka namba ya kumbukumbu
Weka namba ya malipo
Weka kiasi
Weka namba ya Siri kukamilisha malipo
Bonyeza 1 kufanya malipo ya AFCS
Utapokea ujumbe kukujulisha ombi lako linashughulikiwa.

m-pesa